

TANGAZO LA SERIKALI NA.. 348 la tarehe 28/8/2015

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA  
(SURA 290)

**SHERIA NDOGO**

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA  
YA MEATU, ZA MWAKA 2015

- |   |   |
|---|---|
| Jina na mwanzo wa kutumika Eneo la matumizi | 1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, 2015 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.   |
| Tafsiri                                     | 2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya Meatu.  |
|   | 3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo,<br><br>“ <i>Ada na Ushuru</i> ” maana yake ni malipo yanayolipwa kwa ajili ya huduma, vibali na leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri.<br><br>“ <i>Afisa Muidhiniwa</i> ” maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.<br><br>“ <i>Halmashauri</i> ” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Meatu.<br><br>“ <i>Mkurugenzi</i> ” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu pamoja na Afisa yoyote atakayeteuliwa kwa wakati huo kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.<br><br>“ <i>Mifugo</i> ” maana yake ni Ng`ombe, Mbuzi, Kondoo pamoja na wanyama wote wafugwao |

*Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za  
Halmashauri ya Wilaya ya Meatu*

---

*Tangazo la Serikali Na. 348 (linaendelea)*

- |   |   |   |
|---|---|---|
| Utozaji<br>wa Ada na<br>ushuru                        | 4 | (1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru kwa ajili ya bidhaa au huduma, vibali na leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri kama zinavyooneshwa katika jedwali la Sheria Ndogo hizi.<br><br>(2) Ada na Ushuru utozwao Chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya kupata huduma na kibali husika isipokuwa ada zilipwazo kwa muda maalum.<br><br>(3) Huduma zitakazotozwa Ada na Ushuru katika Sheria Ndogo hizi ni:-<br>i. Kukodi Mitambo na Magari ya Halmashauri,<br>ii. Kufunga Barabara,<br>iii. Upimaji wa Ardhi na Vibali vya Ujenzi,<br>iv. Maombi ya Kibali cha Kununua Mazao,<br>v. Mazao ya Kilimo,<br>vi. Mifugo Mnadani,<br>vii. Machinjio na Ukaguzi wa Nyama,<br>viii. Kusafirisha Mifugo,<br>ix. Kukusanya Ngozi,<br>x. Kuogesha Mifugo,<br>xi. Mazao ya Misitu,<br>xii. Mazao ya Samaki,<br>xiii. Chumvi katika Eneo la Uzalishaji,<br>xiv. Kukodi Ukumbi wa Halmashauri,<br>xv. Vibanda vya Stendi na Soko Kuu Mwanhuzi,<br>xvi. Meza / Kizimba / Kiwanja katika Soko,<br>xvii. Matangazo ya Biashara,<br>xviii. Matangazo mengine,<br>xix. Usajili wa Vyombo vya Usafiri,<br>xx. Maegesho ya Magari Mwanhuzi,<br>xxi. Maegesho ya Magari katika Minada na Magulio,<br>xxii. Minada na Magulio,<br>xxiii. Maombi ya Kibali cha Utamaduni na Michezo,<br>xxiv. Shughuli za Utamaduni na Michezo, na<br>xxv. Huduma nyinginezo. |
| Wajibu wa<br>kulipa Ada<br>na Ushuru                  | 5 | Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayestahili kulipa ada au ushuru utozwao kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kuhakikisha kwamba analipa ada au ushuru kama ilivyoelekezwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi..   |
| Ada na<br>Ushuru<br>kulipwa<br>kwa<br>Halmasha<br>uri | 6 | (1) Ada na Ushuru unaotowza kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, utalipwa kwa Halmashauri au Wakala ambaye atatoa stakabadhi kama kielelezo cha kupokea malipo hayo.  |

*Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za  
Halmashauri ya Wilaya ya Meatu*

---

*Tangazo la Serikali Na. 348 (linaendelea)*

- (2) Hautakuwa ni utetezi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi mtu yeyote kudai kuwa amelipa ada au ushuru lakini hakupewa stakabadhi.
- Ukusanyaji wa madeni 7
- (1) Endapo mtu yeyote anayetakiwa kulipa ada au ushuru atashindwa kulipa ada au ushuru huo ndani ya muda uliowekwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Halmashauri inaweza kukusanya ada au ushuru huo kwa njia ya Mahakama.
- (2) Bila ya kuathiri masharti yaliyowekwa na kifungu cha (1) hapo juu, Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ada au ushuru kwa njia ya kukamata na kushikilia mali za mdaiwa zenye thamani sawa na kiasi cha ada au ushuru unaodaiwa.
- (3) Endapo mdaiwa hutakomboa mali zake baada ya siku thelathini kupita tangu kukamatwa kwa mali hizo Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziua kwa njia ya mnada.
- (4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuuza mali hizo kabla hazijaharibika baada ya kuomba na kupata kibali cha Mahakama.
- (5) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuuza mali zilizokamatwa na kushikiliwa ambazo haziharibiki baada ya Mkurugenzi kutoa taarifa ya kusudio la kuuza mali hizo kwa maandishi ndani ya siku nane na endapo mwenye mali atashindwa kulipa deni analodaiwa Halmashauri itaendelea na utaratibu wa kuuza mali hizo.
- (6) Endapo mwenye mali inayoshikiliwa atajitokeza atatakiwa kulipa deni la ada au ushuru analodaiwa, gharama za utunzaji wake pamoja na faini ya asilimia hamsini ya ushuru anaodaiwa na atapewa stakabadhi.
- Halmashauri kutowajibika kwa hasara 8
- Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote na kwa namna yoyote ile itakayotokea aidha wakati wa kukusanya madeni au kwa mali zitakazokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri.
- Uwezo wa Afisa Muidhini wa Makosa na Adhabu 9
- Bila ya kuathiri masharti mengineyo yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi Afisa Muidhiniwa anaweza kuingia katika jengo lolote na mahali popote wakati wa saa za kazi kwa nia ya kukusanya ada au ushuru.
- 10
- (1) Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo mtu yeyote;
- (a) Atakataa au atashindwa kutii agizo lolote atakalopewa na Afisa Muidhiniwa;

*Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za  
Halmashauri ya Wilaya ya Meatu*

---

*Tangazo la Serikali Na. 348 (linaendelea)*

- (b) Atamzuia kwa namna yoyote ile Afisa Muidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;
- (c) Atakataa au kujaribu kukataa kulipa ada au ushuru anaopaswa kulipa;
- (d) Atamshawishi mtu yeyote au kundi la watu kukataa kulipa ada au ushuru;

(2) Mtu yeyote atakayetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi na kutiwa hatiani atalipa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi mitatu jela au vyote viwili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa 11 Mkurugenzi anaweza kumtoza faini isiyopungua shilingi Eflu Hamsini (50,000) mtu yeyote aliyetenda kosa na kukiri kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum iliyoambatanishwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

GN. No. 12 Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Meatu za mwaka 2000 zimefutwa.

373,374,  
375,376,3  
77,378.37  
9,380,383,  
384,385,3  
86,387,38  
8,389,390  
& 392 za  
mwaka  
2000 la  
tarehe  
6/10/2000

*Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za  
Halmashauri ya Wilaya ya Meatu*

---

*Tangazo la Serikali Na. 348 (linaendelea)*

**JEDWALI LA KWANZA**

**VIWANGO VYA ADA NA USHURU**  
*(Chini ya kifungu cha 4(1) cha Sheria Ndogo hizi)*

**SEHEMU I: UJENZI NA MIUNDOMBINU**

**1. ADA ZA KUKODI MAGARI NA MITAMBO YA HALMASHAURI**

<b>Na</b>	<b>Gari/Mitambo</b>	<b>Kiasi cha Ada</b>
1	Magari Makubwa (Malori tani 7 au zaidi) bila mafuta	Sh. 2,000/= kwa kilometa
2	Magari madogo – Bila mafuta	Sh. 1,000/= kwa kilometa
3	Mitambo	
	(a) D6 bila mafuta	Sh. 950,000/= kwa siku
	(b) Greda (Motor grader) bila mafuta	Sh. 950,000/= kwa siku
	(c) Kijiko (Wheel Loader) bila mafuta	Sh. 750,000/= kwa siku
	(d) Trekta bila mafuta	Sh. 80,000/= kwa siku

**2. ADA YA KUFUNGA BARABARA**

<b>Na</b>	<b>Aina ya Shughuli</b>	<b>Kwa siku</b>
1	Harusi na sherehe mbalimbali	Sh.10,000/=
2	Kupitisha bomba kukatisha barabara	Sh.10,000/=

**SEHEMU YA II: ARDHI**

**ADA YA UPIMAJI WA ARDHI NA VIBALI VYA UJENZI**

<b>A. Ada ya Kibali cha Ujenzi/ Upimaji</b>	<b>Kwa kila kibali</b>
1. Mnara wa simu	Sh. 500,000/=
2. Ghorofa moja	Sh. 120,000/=
3. Nyumba za Biashara	Sh. 100,000/=
4. Nyumba ya Makazi yaliyopimwa	Sh. 20,000/=
5. Kituo cha mafuta.	Sh. 200,000/=
6. Majengo ya Taasisi Binafsi.	Sh. 100,000/=
7. Maghala na Bohari.	Sh. 100,000/=

*Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za  
Halmashauri ya Wilaya ya Meatu*

---

*Tangazo la Serikali Na. 348 (linaendelea)*

<b>B. Ada na mabadiliko (alteration) ya jengo lililopo</b>	<b>Kwa kila kibali</b>
1. Nyumba ya kuishi na biashara	Sh. 20,000/=
2. Nyumba ya Biashara.	Sh. 50,000/=
3. Nyumba ya kuishi	Sh. 10,000/=
4. Ghorofa.	Sh. 200,000/=
5. Kiwanda, Bohari, Ghala.	Sh. 100,000/=
6. Mabadiliko ya matumizi ya ardhi (Makazi)	Sh. 50,000/=
7. Mabadiliko ya matumizi ya ardhi (Biashara)	Sh. 100,000/=

  

<b>C. Ada za huduma ya Ardhi</b>	
1. Hati halisi ya Hati Miliki(Original R/O)	Sh. 5,000/= kwa nakala
2. Utafiti wa kitaalum (Official search)	Sh. 5,000/= kwa kila huduma
3. Kubadili Hati Miliki (Transfer of R/O)	Sh. 5,000/= kwa kila moja
4. Mchoro wa upimaji	Sh. 10,000/= kwa kila mchoro
5. Kutambua eneo (Plot identification)	Sh. 10,000/= kwa kila plot
6. Kurudishia mawe yanaonesha mipaka (Beacon replacement)	Sh. 5,000/= kwa kila jiwe

**SEHEMU III: KILIMO**

**1. ADA YA MAOMBI YA KIBALI CHA KUNUNUA MAZAO**

<b>Na. Aina ya Mazao</b>	<b>Kwa Kibali</b>
1 Kununua Pamba	Sh 150,000/=
2 Kununua Mazao mchanganyiko	Sh. 10,000/=

**2. USHURU WA MAZAO YA KILIMO**

<b>Na. Aina ya Mazao</b>	<b>Kiasi cha Ushuru</b>
1 Pamba	Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko
2 Mahindi	Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko
3 Mpunga	Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko
4 Karanga	Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko
5 Mchele	Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko
6 Kunde	Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko

*Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za  
Halmashauri ya Wilaya ya Meatu*

---

*Tangazo la Serikali Na. 348 (linaendelea)*

7	Choroko	Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko
8	Ulezi	Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko
9	Uwele	Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko
10	Mbaazi	Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko
11	Dengu	Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko
12	Maharage	Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko
13	Mbegu za mafuta(Cotton Oil)	Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko
14	Alizeti	Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko
15	Ufuta	Asilimia 5 ya bei ya mauzo ya soko

**SEHEMU IV: MIFUGO**

**1. USHURU WA MIFUGO MNADANI**

<b>Na</b>	<b>Aina ya Mifugo</b>	<b>Kiasi cha Ushuru</b>
1	Ng'ombe	5,000/=
2	Ngamia	5,000/=
3	Mbuzi	1,500/=
4	Kondoo	1,500/=
5	Nguruwe	1,500/=
6	Punda	1,500/=
7	Farasi	1,500/=

*Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za  
Halmashauri ya Wilaya ya Meatu*

---

*Tangazo la Serikali Na. 348 (linaendelea)*

**2. ADA YA MACHINJIO NA UKAGUZI WA NYAMA**

<b>Na.</b>	<b>Aina ya Mnyama</b>	<b>Ada ya Machinjio</b>	<b>Ada ya Ukaguzi</b>	<b>JUMLA</b>
1	Ng'ombe	Sh. 1,500/=	Sh. 1,500/=	3,000/=
2	Mbuzi	Sh. 500/=	Sh. 1,000/=	1,500/=
3	Kondoo	Sh. 500/=	Sh. 1,000/=	1,500/=

**4. USHURU WA KUSAFIRISHA MIFUGO**

<b>Na</b>	<b>Aina ya Mifugo</b>	<b>Ndani ya Wilaya</b>	<b>Nje ya Wilaya</b>	<b>Nje ya Mkoa</b>
1	Ng'ombe	1,000/=	1,500/=	2,500/=
2	Ngamia	1,000/=	1,500/=	2,500/=
3	Mbuzi	500/=	500/=	1,500/=
4	Kondoo	500/=	500/=	1,500/=
5	Nguruwe	500/=	500/=	1,500/=
6	Punda	500/=	500/=	1,500/=
7	Farasi	500/=	500/=	1,500/=

**5. USHURU WA KUKUSANYA NGOZI**

<b>Na.</b>	<b>Aina ya Ngozi</b>	<b>Kiasi cha Ushuru</b>
1	Ngozi ya Ng'ombe	Sh. 300/= kwa kila ngozi inayouzwa
2	Ngozi ya Mbuzi au kondoo	Sh.150/= kwa kila ngozi inayouzwa

**6. ADA YA UOGESHAJI MIFUGO**

<b>Na.</b>	<b>Aina ya Mifugo</b>	<b>Kiasi cha Ada kwa kila Mnyama</b>
1.	Ng'ombe	Sh. 300/=
2.	Mbuzi	Sh. 200/=
3.	Kondoo	Sh. 200/=



*Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za  
Halmashauri ya Wilaya ya Meatu*

---

*Tangazo la Serikali Na. 348 (linaendelea)*

**SEHEMU V: MALIASILI**

**1. USHURU WA MAZAO YA MISITU**

<b>Na.</b>	<b>Aina ya Zao</b>	<b>Kipimo</b>	<b>Kiasi cha Ushuru</b>
1	Mbao	mbao moja	Sh. 50/=
2	Kuni	Mkokoteni 1 ujazo (m <sup>3</sup> 4)	Sh. 1,000/=
3	Mkaa	Gunia moja (kilo 50)	Sh. 4,500/=
4	Miche ya matunda	Moja	Sh. 100/=
5	Miche ya uzio (Fence)	Moja	Sh. 100/=
6	Gundi/Utomvu	Kilo moja	Sh. 100/=
7	Ubuyu	Gunia kilo 28	Sh. 1,000/=
8	Asali	Lita moja	Sh. 300/=
9	Nta	Kilo moja	Sh. 300/=
10	Mizizi/Madawa yatokanayo na miti	Kilo moja	Sh. 100/=

**2. USHURU WA MAZAO YA SAMAKI**

<b>Na</b>	<b>Aina ya Zao</b>	<b>Kiasi cha Ushuru</b>
1	Leseni ya uvuvi	Sh. 20,000/= kwa mwaka
2	Leseni ya chombo	Sh. 50,000/= kwa mwaka
3	Samaki	Sh. 100/= kwa kilo moja
4	Dagaa	Sh. 1,000/= kwa gunia (kilo 100)

**3. USHURU WA CHUMVI KATIKA ENEO LA UZALISHAJI**

<b>Na.</b>	<b>Aina ya Ngozi</b>	<b>Kwa kilo moja</b>
1	Chumvi laini (unga)	Sh. 2,000/= kwa gunia (kilo 150)
2	Chumvi mawe	Sh. 2,000/= kwa gunia (kilo 150)

**SEHEMU VI: BIASHARA**

**1. ADA YA KUKODI KUMBI ZA HALMASHAURI**

<b>Na.</b>	<b>Ukumbi</b>	<b>Kwa kila Kikao</b>
1	Kukodi Ukumbi Mkubwa (mpya)	Sh. 100,000/=
2	Kukodi Ukumbi Mdogo (wa zamani)	Sh. 50,000/=

*Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za  
Halmashauri ya Wilaya ya Meatu*

---

*Tangazo la Serikali Na. 348 (linaendelea)*

**2. USHURU WA VIBANDA VINAVYOZUNGUKA STENDI NA SOKO KUU MWANHUZI**

<b>Na.</b>	<b>Eneo</b>	<b>Kiasi cha Ushuru</b>
1	Vibanda vya mzunguuko wa Ndani ya Soko	Sh. 120,000/= kwa mwaka
2	Vibanda vya mzunguuko wa Nje ya Soko	Sh. 180,000/= kwa mwaka
3	Sehemu iliyopimwa kwa ajili ya Kituo cha biashara au stendi	Sh. 120,000/= kwa mwaka

**3. USHURU WA MEZA/VIZIMBA KATIKA SOKO**

<b>Na.</b>	<b>Eneo</b>	<b>Kiasi cha Ushuru</b>
1	Masoko ya Mwanhuzi (Eneo la Meza moja)	Shs 6,000/= kwa mwezi au 200/= kwa siku
2	Masoko Mengineyo (Eneo la Meza moja)	Shs 3,000/= kwa mwezi au 100/= kwa siku

**4. USHURU WA MBAO ZA MATANGAZO YA BIASHARA**

<b>Na</b>	<b>Aina ya tangazo</b>	<b>Kiwango cha Ushuru</b>
1.	Maombi ya kuweka mabango ya Biashara / kuchora	Sh. 3,000/= kwa maombi
2.	Matangazo kwenye mabango yanayong'aa	Sh. 15,000/= kwa meta za eneo
3.	Matangazo kwenye mabango yasiyong'aa	Sh. 10,000/= kwa meta za eneo
4.	Matangazo kwenye kuta za nyumba (yanayong'aa)	Sh. 6,000/= kwa meta za eneo
5.	Matangazo kwenye kuta za nyumba (yasiyong'aa)	Sh. 4,000/= kwa meta za eneo
6.	Matangazo kwa kutumia Kitambaa	Sh. 5,000/= kwa mwezi/tukio
7.	Kibali cha Matangazo ya vipaza Sauti/ Magari na Promosheni	Sh. 10,000/= kwa kibali

**5. ADA YA USAJILI WA VYOMBO VYA USAFIRI**

<b>Na.</b>	<b>Aina ya Chombo cha Usafiri</b>	<b>Kwa mwaka</b>
1	Mabasi madogo (hadi abiria – 30)	Sh. 15,000/=
2	Mabasi makubwa	Sh. 50,000/=
3	Malori madogo (chini ya tani 7)	Sh. 20,000/=
4	Malori makubwa (zaidi ya tani 7)	Sh. 30,000/=
5	Teksi	Sh. 10,000/=
6	Pikipiki za Biashara (Bodaboda)	Sh. 5,000/=

*Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za  
Halmashauri ya Wilaya ya Meatu*

---

*Tangazo la Serikali Na. 348 (linaendelea)*

**6. USHURU WA MAEGESHO - MWANHUZI MJINI**

<b>Na.</b>	<b>Aina ya Chombo cha Usafiri</b>	<b>Kwa siku</b>
1	Teksi	Sh.1,000/=
2	Mabasi yanayofanya safari ndani ya Wilaya	Sh.2,000/=
3	Mabasi yanayofanya safari nje ya Wilaya	Sh.5,000/=
4	Lori tani 8 – 12	Sh.2,000/=
5	Lori tani 13 na kuendelea	Sh.5,000/=
6	Lori chini ya Tani 8	Sh.2,000/=
7	Magari madogo yanayofanya safari nje ya Wilaya	Sh.2,000/=
8	Magari madogo yanayofanya biashara ya kubeba abiria	Sh.1,000/=

**7. USHURU WA MAEGESHO – MAENEO YA MINADA NA MAGULIO**

<b>Na.</b>	<b>Aina ya Chombo cha Usafiri</b>	<b>Kwa siku ya Mnada / Gulio</b>
1	Magari makubwa ya Mizigo	Sh.3,000/=
2	Magari madogo ya Mizigo	Sh.1,000/=

**8. USHURU WA MINADA NA MAGULIO**

<b>Na.</b>	<b>Aina ya Biashara</b>	<b>Kwa siku ya Mnada / Gulio</b>
1	Kiwanja kimoja cha Biashara	Sh. 1,000/=
2	Baba / Mama Lishe	Sh. 500/=
3	Kupakia mifugo katika Lori – Ng’ombe	Sh. 5,000/=
4	Kupakia mifugo katika Lori – Mbuzi & Kondoo	Sh. 5,000/=

**SEHEMU VII: UTAMADUNI NA MICHEZO**

**1. ADA YA MAOMBI YA KIBALI CHA UTAMADUNI NA MICHEZO**

<b>Na.</b>	<b>Aina ya Mchezo</b>	<b>Kwa Kibali</b>
1	Shughuli zote za Utamaduni na Michezo	Sh. 5,000/=

*Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za  
Halmashauri ya Wilaya ya Meatu*

---

*Tangazo la Serikali Na. 348 (linaendelea)*

**2. ADA ZA SHUGHULI ZA UTAMADUNI NA MICHEZO**

<b>Na.</b>	<b>Aina ya Shughuli</b>	<b>Kiasi cha Ada</b>
1	Kupiga muziki wa Dansi	Sh. 20,000/= kwa siku
2	Mazingaombwe	Sh. 10,000/= kwa siku
3	Ngoma za jadi	Sh. 15,000/= kwa ngoma
4	Kutumia kiwanja cha michezo	Sh. 20,000/= kwa siku
5	Kutumia kiwanja cha michezo kwa shughuli isiyo ya kiingilio	Sh. 2,000/= kwa siku
6	Kuonyesha sinema, video yenye kiingilio	Sh. 5,000/= kwa siku
7	Ada ya kibali cha kuonyesha sinema au video isiyo ya kiingilio	Sh. 2,000/= kwa siku
8	Michezo ya sanaa za maonyesho, ngoma, maigizo, sarakasi, michezo ya ngumi na nyimbo	Sh. 5,000/= kwa siku
9	Kufanya shughuli za sanaa za ufundi (uchoraji) picha, upakaji rangi, uchongaji mihuri na vinyago	Sh. 2,000/= kwa siku
10	Kunasa sauti kwa vikundi wakati wa mashindano ama shughuli iliyoandaliwa na Halmashauri	Sh. 2,000/= kwa siku
11	Vikundi vya sanaa za maonyesho na sanaa za ufundi	Sh. 5,000/= kwa siku
12	Kufanya matangazo ya biashara katika Bar/Hotel	Sh. 10,000/= kwa siku
13	Kufanya matangazo ya biashara katika maeneo ya wazi	Sh. 30,000/= kwa siku
14	Kuonesha ngumi, mieleka au Kungfu	Sh. 10,000/= kwa siku
15	Kuchezesha mchezo wa Pool (Pool Table)	Sh. 5,000/= kwa mwezi
16	Usambazaji wa Cable za Luninga (TV)	Sh. 10,000/= kwa mwezi
17	Usajili wa shughuli za Utamaduni	Sh. 10,000/= kwa mwaka

**3. ADA NA USHURU MWINGINE**

<b>Na.</b>	<b>Chanzo</b>	<b>Kiasi cha Ada / Ushuru</b>
1	Usajili wa Vikundi vya Uzalishaji Mali	Sh. 20,000/= kwa kikundi
2	Usajili wa Klabu za usiku (Night Club)	Sh. 50,000/= kwa mwaka

*Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za  
Halmashauri ya Wilaya ya Meatu*

*Tangazo la Serikali Na. 348 (linaendelea)*

JEDWALI LA PILI

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MEATU**



**HATI NA.** .....

**Tarehe**.....

**FOMU YA MAOMBI YA KIBALI CHA KUNUNUA MAZAO MCHANGANYIKO**  
(Ijazwe na mwombaji)

1. Jina la Mnunuzi/mwenye Kampuni / Ushirika .....
2. Jina la Kampuni/Shirika/Mnunuzi.....
3. Anuani yake S.L.P..... Simu..... Wilaya.....
4. Mahali Ofisi yake ilipo; Mtaa..... Kata..... Wilaya.....
5. Mahali anapoishi/mji..... Mtaa.....
6. Namba ya leseni ya Biashara.....
7. Namba ya kuandikishwa Shirika/Kampuni.....
8. Mazao anayotaka kununua Kilo.....
9. Kiasi anachotaka kununua (idadi ya Kilo).....
10. Maeneo/vijiji atakaponunua.....
11. Idadi na mahali yalipo maghala atakayotumia kuhifadhia mazao yake:  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....

Dhamana alizoweka:

1. ....
2. ....

**NATHIBITISHA:** Kuwa maelezo yote niliyotoa hapo juu ni sahihi na kweli.

1. Jina la mwombaji.....
2. Sahihi ya mwombaji.....
3. Tarehe.....
4. Mhuri.....

Nakala ya kibali itunzwe kwa ajili ya ukaguzi wakati wowote:

Nakala ya kibali hiki itabaki kwa:

1. Mkuu wa Wilaya ya Meatu
2. Afisa Mtendaji wa kijiji cha .....
3. Afisa Mtendaji kata ya .....

\_\_\_\_\_  
Mkurugenzi Mtendaji (W)  
**MEATU**

*Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za  
Halmashauri ya Wilaya ya Meatu*

*Tangazo la Serikali Na. 348 (linaendelea)*

JEDWALI LA TATU

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MEATU**



**HATI NA. ....**

**Tarehe.....**

**FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA**

*(Chini ya kifungu cha 11 cha Sheria ndogo hizi)*

Mimi .....

Nakiri mbele ya .....ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, kwamba mnamo tarehe ..... ya Mwezi ..... Mwaka ..... nilitenda kosa la kukiuka maelekezo ya kifungu cha ..... cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Meatu (Ada na Ushuru) za Mwaka 2011; sasa nipo tayari kulipa faini kiasi cha Sh.....ikiwa Mkurugenzi ataamua kutekeleza mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 11 cha Sheria Ndogo hizi.

Nathibitisha kwamba maelezo niliyotoa ni ya kweli nimeyatoa kadri ya ufahamu wangu leo tarehe.....Saini.....

**AFISA MUIDHINIWA**

Nimepokea kiasi cha Sh..... toka kwa mtajwa hapo juu na nimemkatia risiti namba.....

Jina: .....

Cheo: .....

Saini: .....

*Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za  
Halmashauri ya Wilaya ya Meatu*

*Tangazo la Serikali Na. 348 (linaendelea)*

JEDWALI LA NNE

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MEATU**



**HATI NA. ....**

**Tarehe.....**

**HATI YA KUKAMATA NA KUUZA MALI**

*(Chini ya kifungu cha 7(2) cha Sheria Ndogo hizi)*

**KWA DALALI WA MAHAKAMA**

.....  
.....  
.....

Hii ni kukuamuru kukamata na kuitunza mali inayoondosheka ya .....  
..... ambayo imeonyeshwa katika jedwali, mpaka hapo  
mtajwa hapo juu atakapolipa Tsh..... zikiwa ni deni  
la ada au ushuru analodaiwa pamoja na riba kwa kiwango cha ..... kila mwezi  
kuanzia tarehe.....mwezi ..... mwaka ..... ikiwa ni pamoja na gharama za  
kukamata na kutunza mali hiyo. Mauzo ya mali hiyo yatafanywa kwa mnada ili kupata Shs  
..... pamoja na riba na gharama za kukamata na kutunza mali hiyo.

Unaamriwa kurudisha hati hii mnamo au kabla ya tarehe ..... mwezi ..... mwaka  
..... pamoja na maelezo ya namna ulivyotekeleza amri hii au sababu ya kwa nini hukutekeleza.

**Imetolewa na Mimi** ..... na kugongwa mhuri wa mahakama  
leo tarehe ..... mwezi ..... mwaka 20.....

\_\_\_\_\_  
**HAKIMU**

*Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za  
Halmashauri ya Wilaya ya Meatu*

---

*Tangazo la Serikali Na. 348 (linaendelea)*

Muhuri Rasmi wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu ulibandikwa katika Sheria ndogo hizi kufuatia azimio la Halmashauri lililopitishwa kwenye mkutano wa kawaida uliofanyika Tarehe.....Mwezi..... 2015 na muhuri huo wa Halmashauri uliwekwa mbele ya:-

Pius. Z. Machungwa  
**Mwenyekiti wa Halmashauri.**

Godfrey B. Machumu  
**Mkurugenzi wa Halmashauri**

**NAKUBALI,**

**Dodoma**

MHE. MIZENGO K. P. PINDA (MB.),

Tarehe.....Mwezi.....2015

Waziri mkuu